



TANGAZO LA KAZI KWA NAFASI YA FUNDI RANGI (Maalumu kwa vyuma)

BESIX Ballast Nedam (BBN) Limited, ni MKANDARASI anayehusika na uhandisi, ununuzi na ujenzi wa gati na kituo cha kupakia mafuta ghafi ya mradi wa EACOP, anakaribisha maombi kwa nafasi ya kazi ya Fundi Rangi (Maalumu kwa vyuma).

Mradi	EACOP – Jetty & Loading Out Facility
Muajiri	BESIX Ballast Nedam Limited (BBN)
Mahali pakazi	Tanga
Nafasi ya kazi	Fundi Rangi (Maalumu kwa vyuma)
Mkuu wa Idara:	Meneja Ujenzi
Kipindi cha kazi	December 2023 – May 2025

Dhumuni la kazi

Fundi rangi atakua na jukumu la kupaka rangi kwa kiwango cha hali ya juu katika vyuma na vifaa vingine ambavyo vinatumika katika sekta ya mafuta na gesi. Fudi rangi atapaka rangi katika maeneo na mazingira tofauti tofauti kwakutumia mashine za kisasa za kupuliza rangi.

Majukumu ya kazi

- Kutunza vifaa vya kazi.
- Kuandaa eneo la kupulizia rangi kwa kutumia maji kusafisha, kuparaza kwa mashine na/au kwa njia nyinginezo.
- Kuandaa mashine ya kupulizia rangi.
- Kupulizia rangi kwa kutumia njia tofauti tofauti kama vile Manuel na Vacuum.
- Kuhakikisha rangi yote inapulizwa au kupakwa kwa kuzingatia viwango husika vya sekta na pia kanuni mbalimbali kama vile NACE na SSPC.
- Kuwa na ujuzi wa kutosha na pia uthibitisho toka kwa taasisi maalumu za rangi kama vile AMPP, NACE na FROSIO.
- Kutunza vyema kumbukumbu za kazi iliyofanyika na pia vifaa vilivyotumika.
- Kuwasiliana na wafanyakazi wenzako na pia viongozi wako ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi.

Sifa za muombaji.

Muombaji awe na sifa zifuatazo:

- Awe raia wa Tanzania
- Elimu ya Diploma au taaluma nyingine yeyote husika kwa kazi hii.
- Vyeti vya mafunzo muhimu kwa kazi ya rangi



- Angalau uzoefu usiopungua miezi mitatu kwa kazi ya rangi hasa katika sekta ya mafuta na gesi.
- Ufahamu wakutosha kuhusu viwango stahiki katika sekta ya rangi kama vile NACE na SSPC.
- Uwezo wa kusoma na kuelewa michoro na maelekezo ya kitaalamu.
- Uzoefu wa kutumia vifaa na namna tofauti tofauti za kupaka rangi kama vile Manuel na Vacuum.
- Umahiri na umakini wa kuzingatia maelekezo na viwango vya ubora.
- Uwezo wa kufanya kazi kwa kushirikiana.
- Uwezo wa kufanya kazi katika hali zote na pia maeneo ya ndani na ya nje.
- Utayari wa kufanya kazi muda tofauti tofauti ikiwa ni pamoja na usiku au siku za mwisho wa wiki pale inapohitajika.

Jinsi ya kutuma maombi:

Maombi yote yatapokelewa kupitia email address jobs@bbnltd.co.tz na mwisho wa kupokea maombi haya ni 20 December 2023.

Jinsi ya kutuma maombi:

Anuani kwaajili ya maombi ya kazi ni: **Meneja Mradi, BESIX Ballast Nedam Ltd. TANGA.** Maombi yote yatapokelewa kupitia ofisi ya kata ya Chongoleani au barua pepe jobs@bbnltd.co.tz na mwisho wa kupokea maombi haya ni 20 Desemba 2023.

Kwa maswali/maelekezo;- +255 747 958 460 (ndani ya muda wa kazi, saa 1:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni, Jumatatu hadi Jumamosi)

ZINGATIA. *Kwa nafasi hii, waombaji kutoka maeneo mengine ya Tanzania hawatakiwi kupiga muhuri barua zao za maombi katika Ofisi ya Kata ya Chongoleani, Ni wazawa wa kata ya Chongoleani pekee wanaostahili kufanya hivyo.*

HAKUNA AJIRA MLANGONI!!! USITOE HELA KUPATA KAZI!!!

TAMBUA KUWA, endapo hatutawasiliana na wewe wiki mbili baada ya tarehe ya mwisho ya tangazo hili, maombi yako yatakuwa hayajafanikiwa.